

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI)
SHULE YA SEKONDARI SHUME
S.L.P 197 LUSHOTO.

MAAGIZO YA WANAFUNZI WANAOJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

JINA

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Shume kidato cha kwanza kwa mwaka 2021.

Tafadhali zingatia maelezo yafuatayo:-

1. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021. Zingatia kuwa ratiba ya masomo itaanza rasmi siku ya Jumatatu asubuhi tarehe 11.01.2021. Ni muhimu sana kufika shuleni siku hiyo ili kupisha ratiba ya masomo kuanza kwa wakati. Usiporipoti kwa wakati husika nafasi yako itafutwa.

2. SARE YA SHULE

WAVULANA:

- Suruali mbili rangi ya Nyeusi zisizobana.
- Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi na vya kufunga kwa kamba
- Soksi nyeupe pea mbili au zaidi.
- Mkanda wa suruali mweusi.
- **Sweta rangi ya Kijani moja au zaidi.**

WASICHANA

- Sketi mbili rangi ya Kijani linda box , belt ya wastani, ndefu kuvuka goti.
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi.
- Soksi nyeupe pea mbili au zaidi.
- Hijabu nyeupe mbili za kushona (**kwa wanaovaa tu**) isiyo na marembo.
- **Sweta rangi ya Kijani moja au zaidi**

3. NGUO ZA MICHEZO

- Raba za michezo pea moja.
- Track suti (suruali ya michezo) nyeusi kwa wavulana yenye ufito mweupe na Track suti ya bluu kwa wasichana yenye ufito mweupe.

TANBIHI/MUHIMU:

Zingatia kwa makini maagizo ya sare ya shule kwa kulinda maadili na nidhamu ya shule pia sare ni lazima iwe mpya.

4. VIFAA VYA TAALUMA

- Daftari 11 counters book kwaya two au zaidi.
- Mkebe (mathematical set) 1.
- Rula moja.
- Kalamu za wino , penseli, kifutio, rangi za kuchorea.
- Vitabu vya ziada na kiada (kama vipo)
- Kamusi (Dictionary) ya kiingereza kwa kiingereza (ni muhimu)

5. VIFAA VYA USAFI

- Ndoo ndogo moja kwa wasichana tu.
- Ndoo kubwa moja kwa wavulana.
- Jembe lenye mpini moja kwa wasichana
- Panga moja kwa wavulana.
- Fagio la chelewa moja kwa wote, wavulana na wasichana.

6. CHAKULA

Kila mwanafunzi anapaswa kuchangia chakula cha mchana kwa mchanganuo ufuatao:-

- ✓ Kilo **12** za Mahindi yaliyokobolewa kwa Muhula.
- ✓ Kilo **5** za Maharage kwa Muhula.
- ✓ Shilingi elfu mbili na mia tisa (**2900**) kwa ajili ya mpishi na viungo kwa muhula wa kwanza yaani **Januari mpaka Juni 2021 tu**

Aidha, usilete **nusu** wala **robo** ya chakula. Lete mahitaji yote ya chakula yaliyotajwa hapo juu kwa wakati mmoja kuepuka usumbufu. **HATUTAPOKEA CHAKULA PUNGUFU. CHAKULA KIJE CHOTE CHA MUHULA MZIMA WA KWANZA.**

Mahindi yasichanganywe na Maharage.

7. FOMU MBALIMBALI

- Fomu ya kupimwa afya mwanafunzi apelekwe hospitalini daktari ampime na kujaza taarifa za afya yake katika fomu hiyo. (Ijazwe kwenye hospitali ya serikali au kituo cha afya)
- NB:Mwanafunzi ahakikishe anafanyiwa vipimo kabla ya kujaziwa fomu ya daktari.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SHUME.

.....
LAWRENT STEPHEN KILAPILO
MKUU WA SHULE - SHUME SEKONDARI

Simu namba :- + 255 653607024 au + 255 622590459

KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE YA SEKONDARI SHUME

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI

- (i) Wizi
- (ii) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
- (iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
- (iv) Makosa mengine ya Jinai.
- (v) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi
- (vi) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
- (vii) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
- (viii) Kuoja au kuolewa.
- (ix) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- (x) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
- (xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
- (xii) Kukataa adhabu halali.
- (xiii) Kujiachisha shule mwenyewe.
- (xiv) Kumiliki simu ya mkononi au kifaa cha mawasiliano ukiwa shuleni.

FOMU YA TAARIFA YA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi
2. Tarehe ya kuzaliwa
3. Jina la mzazi / Mlezi
4. Anuani ya mzazi / Mlezi
5. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi
6. Kijiji Kata.....
7. Shule ya msingi alikotoka.....
8. Saini ya mwanafunzi

9. Kazi ya baba Kazi ya mama
10. Jina la mzazi (a) Baba Hai / amefariki
(b) Mama Hai / amefariki
(c) Mlezi

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyekubaliana na maelezo yote. Naahidi kuwa nitakamilisha taratibu zote za shule kila mwanzo wa muhula bila usumbufu wowote.

Jina Saini Tarehe

Mawasiliano/Namba ya Simu.....

UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI

Mimi naahidi kuwa mwanafunzi mtiifu na kufuata utaratibu wote hapa shuleni na ninapokiuka utaratibu nichukuliwe hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina Saini Tarehe

**GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

SHUME SECONDARY,
P.O.BOX 197
LUSHOTO.

MEDICAL, OFFICER

MR/ _____

Please examine the above named pupil that he/she is physical and mental fit/unfit for full time schooling course

(a) (i) eye sight _____

(ii) Limbs _____

(iii) Speech _____

(v) Venereal disease _____

(vi) Leprosy _____

(vii) Epilepsy _____

(b) Neuroses _____

(c) Other serious disease (**mention**)

Pregnant test _____

Other important test (**if any**) _____

Station _____ Name _____ Signature _____

Designation _____